JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA

SHULE YA SEKONDARI AZANIA

Simu: +255 719 999 830
Barua pepe :info@azaniasecondary.sc.tz
headmaster@azaniasecondary.sc.t
Tovuti : http://www.azaniasecondary.sc.tz

Ofisi ya Mkuu wa Shule,
S.L.P 9074,
Dar es salaam.
Upanga Magharibi

Kumb. Na. AZ/SG.13 /VOL.VII /____ 16 Desemba, 2016

Jina la Mwanafunzi .....

S.L.P.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI AZANIA WILAYA ILALA MKOA WA DAR ES SALAAM MWAKA 2017

1. UTANGULINZI:

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha I katika shule hii mwaka 2017.Shule ya Sekondari ya Azania ipo umbali wa km.....kaskazini/mashariki/magharibi/kusini mji mkuu wa Mkoa /Halmashauri ya .....Usafiri wa basi kutoka mjini .....unapatikana katika kituo cha mabasi cha .....Nauli ni T.sh .....

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 09/01/2017,unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 02/01/2017 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 23/01/2017 ndani ya siku saba.

2. MAHALI SHULE ILIPO:

Shule hii ipo katika Barabara ya Umoja wa Mataifa karibu na kituo cha **ZIMAMOTO** (**FIRE**) **KATI YA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA JANGWANI NA** Hospitali Taifa ya Muhimbili.

3. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

A. (i) Sare ya shule ni **suruali ya rangi ya Daki Bluu** (Dark Blue) ,**marinda**

mawili ,(Turn up) na upana chini (**inchi 17)** na **Shati jeupe la mikono mifupi jozi mbili(2)**

(ii) **Viatu vyeusi vya ngozi visivyochongoka** vya kamba, siyo raba nyeusi.

(iii) **Soksi nyeusi** na **mkanda mweusi** wenye kichuma cha kawaida cha kufungia.

4. MAHITAJI MENGINE YA MWANAFUNZI:

(i) Madaftari makubwa
(ii) Mathematics Set (Mkebe wa Hesabu)
(iii) Kalamu za Wino na Penseli
(iv) Rula na kifutio
(v) Vitabu vya masomo- mbalimbali- pata ushauri toka kwa mwalimu/Idara husika
(vi) Begi la kubebea vifaa vyake.

5. RATIBA YA SHULE huanza **Saa 1.00 asubuhi** hadi **saa 8.30 mchana**.

NB: **RATIBA YA SIKU ZA IJUMAA huanza saa 1.00 asubuhi** na kuishia **saa 6.00 mchana** ili kuwawezesha **Wanafunzi wa Kiislamu** kuhudhuria **SWALA YA IJUMAA.**

6. MASOMO YANAYOFUNDISHWA:

(i) Mwanafunzi wa kidato cha kwanza na cha pili analazimika kusoma **masomo kumi na mawili** (**12**) ya lazima ambayo ni: **Basic Mathematics, English, Kiswahili History, Geography, Civics, Physics, Chemistry,Biology, Dini na masomo ya Biashara "Commerce" na "Book- Keeping**" na **somo moja tu la hiari kati** ya haya yafuatayo: **French, Fine Arts, Additional Mathematics, Islamic Knowledge, Bible Knowledge, Physical Education and Computer"**

(ii) Mwanafunzi wa **Kidato cha Tatu** na **Kidato cha Nne** atasoma masomo ya Mchepuo wa:

(a**)** **Sayansi** wenye masomo ya **Basic Mathematics, English, Kiswahili,Civics, Biology**, **Geograpy,Physics, Chemistry,History, Dini** na **somo moja la hiari.**

(b) Sanaa ambayo ni : **Basic Mathematics ,English, Kiswahili, Biology,Civics, History, Geography ,Dini** na **somo moja la Hiari.**

(c) Biashara ambayo ni **"Commerce" na " Book-Keeping**" pamoja na masomo yote ambayo yametajwa katika **6(ii)-b**

NB: Uwezo wake kitaaluma ndio utakaomfanya awe kundi lipi. Kipimo ni matokeo ya **Mitihani ya Taifa ya Kidato** cha **Pili.**Pia lugha ya mazungumzo awapo mazingira ya Shule ni **ENGLISH.**

7. KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE:

(a) MAHUDHURIO:

Mwanafunzi hana budi kuhudhuria vipindi vyote vya masomo Darasani na siku za masomo kwa mwaka (siku 196) . Mwanafunzi atakayeshindwa kuhudhuria **MBILI YA TATU (2/3**) ya siku hizo **BILA SABABU MAALUMU** atakuwa **AMEJIONDOA** mwenyewe shuleni.

(b) SHERIA ZA SHULE:

* Sare zivaliwe – shati lichomekewe ndani ya suruali, na kufunga mkanda mweusi.
* Shati lazima liwe na **NEMBO** ya shule Kila siku.
* Nywele ziwe fupi- mkato wa kawaida bila mtindo wowote; bwenzi, kipara haviruhusiwi.
* Mwanafunzi hana budi kuwaheshimu au kuwatii watu wote, walimu, wafanyakazi wasio walimu,viongozi na wageni wanaofika Shuleni.
* Kuvaa pete, bangili, mkufu au marembo yoyote hayaruhusiwi.
* Epuka vitendo viovu kama matusi, utoro, wizi, ugomvi, ulevi na pombe, madawa ya kulevya, uvutaji sigara, bangi, uasherati ; ushoga, kuoa, kuchochea migomo na vitu vinginevyo. Kwani makosa haya yanaweza kumfanya mwanafunzi achukuliwe hatua zilizotajwa hapa chini (Kipengele **8** au **9**).
* Timiza wajibu wa kazi uliyopangiwa.
* Usiandike mahali pasipohusika kama vile kutani, vitabuni, kwenye samani nk.
* Usimpige au kumshambulia mwanafunzi mwenzako au hata mtu mwingine yeyote.
* Usikatae uteuzi wa kushiriki shughuli mbalimbali kama vile michezo, maandamano, uwakilishi n.k.
* Usifanye biashara yoyote shuleni
* Usibandike tangazo lolote bila ruhusa ya mwalimu anayehusika kukilea kikundi kinachohusika.
* Usihubiri dini, siasa au jambo lolote. Sala zote zifanyike mahali panapohusika kama vile **Kanisani** au **Msikitini.**

(c) **HATUA ZICHUKULIWAZO KWA KUKIUKA TARATIBU NA SHERIA ZA SHULE:**

* Kuonywa
* Kufanyakazi za mikono zaidi
* Kupigwa viboko
* Kusimamishwa Shule

(d) MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE:

1. Wizi
2. Uasherati
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
4. Uvutaji bangi

5. Makosa ya Jinai
6. Kupigana au kupiga
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
8. Kudharau Bendera ya Taifa
9. Kuoa au kuolewa
10. kusababisha **mimba ndani** na **nje** ya Shule
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani au usalama wa Shule au watu
12. Kukataa adhabu kwa makusudi.

(e) ULINZI WA MALI ZA SHULE NA BINAFSI:

Mwanafunzi lazima awe mlinzi na mtunzaji wa mali zote za Shule na za binafsi.

(f) MENGINEYO:

(a) Ni **marufuku kwa mwanafunzi kuwa na simu** ya kiganjani akiwa ndani wala nje ya darasa. Atakayepatikana na simu adhabu kali itachukuliwa dhidi yake **sanjari na kunyang'anywa hiyo simu** na **KUHARIBIWA papo hapo.**

* Shule itafunguliwa tarehe ----------siku ya ----------

* Kikao cha **Wazazi / Walezi** kitafanyika tarehe ---------- siku ya -------

* Tarehe ya mwisho ya kuripoti Mwanafunzi ni ---------- baada ya tarehe hiyo **HATAPOKELEWA.**

MKUU WA SHULE.
SHULE YA SEKONDARI AZANIA

NAKALA KWA:

: Afisaelimu Wilaya

: Mkurugenzi Manispaa Ilala

: Mkaguzi Mkuu – Kanda ya Dar es salaam.

FOMU YA USAJILI (IJAZWE NA KURUDISHWA SHULENI).

PICHA YA MWANAFUNZI

SEHEMU "A" IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE.

Jina kamili la Mwanafunzi _____
Tarehe ya kuzaliwa_____ (3) Mahali (Wilaya) _____
(4) Uraia _____ (5) Dini_____Dhehebu_____
(6) Shule ya Msingi uliyosoma_____
Namba ya Mtihani PS. _____
(7) Shule ya Sekondari uliyopangwa (FI - IV) _____
(8) Shule ya sekondari uliyotoka (FV) _____
Nambari ya Mtihani S._____
(9) Mahali unapoishi kwa sasa _____

AHADI YA MWANAFUNZI:
Mimi _____ Nakubali nafasi niliyopewa ya Kidato cha **Kwanza / Pili /Tatu / Nne / Tano.**

Naahidi kutii kikamilifu Sheria / Kanuni zote za shule wakati wote niwapo mwanafunzi wa **AZANIA.**

SAHIHI YA MWANAFUNZI_____**TAREHE**_____

SEHEMU B: IJAZWE NA MZAZI / MLEZI:

PICHA YA MZAZI / MLEZI

1. Jina la Mzazi/Mlezi _____
2. Kazi _____
3. Anuani _____
4. Simu _____
5. Mahali ninapoishi_____

AHADI YA MZAZI / MLEZI YA KULIPA KARO / MICHANGO YA SHULE:
Mimi_____Mzazi /Mlezi wa
_____
wa **Kidato cha Kwanza/Pili /Tatu / Nne /Tano mwaka 20**_____ katika **Shule ya sekondari AZANIA**. Nathibitisha na kuahidi kuwa nipo tayari kushirikiana na Shule kwa ajili ya malezi ya mtoto wangu ili kufanikisha maendeleo ya shule na mwanafunzi.

Pia naahidi kuwa kila ifikapo mwisho wa **Muhula wa Shule** (**Mwezi Juni** au **Desemba**) Nitakuwa Nafuatilia ripoti na Matokeo yake kikamilifu

Mimi _____wa S.L.P._____Simu namba _____

SAHIHI YA MZAZI/MLEZI_____ Tarehe_____

FOMU NA 2: FOMU YA TAARIFA YA AFYA YA MWANAFUNZI "MEDICAL EXAMINATION FORM"

Maelezo: Fomu hii ijazwe na Mganga Mkuu wa Mkoa/Wilaya na Mwanafunzi aje nayo shuleni na kuikabidhi ofisi ya nyaraka za wanafunzi.

Mimi [Jina la Mganga Mkuu wa Mkoa/Wilaya]_____

Nathibitisha kuwa Mwanafunzi [Jina la mwanafunzi]_____

Amepimwa nami kikamilifu na kuonekana anayo / hanayo afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo;-

[A] **Hali ya mwili**

[I] Mapigo ya moyo_____

[ii] Haemoglobin;_____

[iii] Kundi la damu[blood group]_____

[iii] Mkojo_____

[iv] Kinyesi_____

[vi] Macho yana kasoro_____

[vii] Masikio yana kasoro_____

Angalia: Weka maoni yako kuhusu kila kilichotajwa (a) (**i**) - (**vii**)

[B] **Magonjwa**

[a] Bronchal asthma_____

[b] Tuberculosis_____

[c] Epilepsy_____

[d] Blood pressure_____

[e] Peptic/deudenal ulcers_____

[f] Sickle cells_____

[g] Ukoma_____

[h] Veneral disease[give type]_____

[I] Mental illness_____

[j] Any other serious disease not mentioned above_____

[k] Foetus_____

Saini ya Daktari _____ **Muhuri**_____ **Tarehe**_____

Futa neno lisilo husika